



TAARIFA KWA UMMA
WATALII WALIOINGIA NCHINI
KIPINDI CHA JANUARI - AGOSTI, 2023



Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822
Barabara ya Jakaya Kikwete
Nukushi: +255 26 296382
S. L. P. 2683
Barua pepe: sg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz
Dodoma - TANZANIA



1.0 Utangulizi

Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina jukumu la kutayarisha na kusambaza takwimu za kijamii na kiuchumi kwa mujibu wa **Sheria ya Takwimu SURA 351**. Miongoni mwa taarifa hizo ni takwimu za mara kwa mara (high-frequency data) za mwenendo wa watalii walioingia Nchini.

2.0 Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Januari - Agosti 2023

Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi walioingia nchini katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2023 waliendelea **kuongezeka hadi 1,131,286** ikilinganishwa na watalii **900,182** walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni **ongezeko la watalii 231,104** sawa na **asilimia 25.7 (Jedwali Na. 1)**. Kati ya watalii wote walioingia nchini katika kipindi hicho, watalii **236,047** waliingia nchini kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia **31.1** ya watalii wote.

3.0 Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Agosti 2023

Watalii walioingia Nchini mwezi Agosti 2023 pekee, **waliongezeka hadi 186,030** ikilinganishwa na watalii **158,049** walioingia nchini mwezi Agosti 2022, sawa na ongezeko la asilimia **17.7**. **Watalii 336,203** kati ya watalii wote walioingia nchini mwezi Agosti 2023, waliingia Nchini kupitia Zanzibar sawa na asilimia **29.7** ya **idadi ya watalii wote (Jedwali Na. 1)**.

Jedwali Na. 1: Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kuanzia Januari hadi Agosti 2023

Mwezi	2022	2023	Ongozeko	Badiliko (%)
Januari	94,441	146,877	52,436	55.5
Februari	101,042	144,019	42,977	42.5
Machi	93,889	118,186	24,297	25.9
Aprili	79,405	96,852	17,447	22.0
Mei	89,271	106,497	17,226	19.3
Juni	117,349	146,896	29,547	25.2
Julai	166,736	185,929	19,193	11.5
Agosti	158,049	186,030	27,981	17.7
Jumla	900,182	1,131,286	231,104	(Jan - Agosti) 25.7

Chanzo: Idara ya Uhamiaji - Septemba, 2023

4.0 Idadi ya Watalii Walioingia Nchini kwa Mchanganuo wa Utaifa, Januari hadi Agosti 2023

4.1 Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kutoka Nje ya Bara la Afrika

Idadi kubwa ya watalii walioingia nchini kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika kwa mchanganuo wa utaifa katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2023 walitoka Marekani ikiwa ni watalii 84,541. Nchi nyingine zilizokuwa na idadi kubwa ya watalii ni: Ufaransa (72,009), Ujerumani (57,798), Uingereza (51,505) na Italia (51,056). Aidha, katika mwezi Agosti 2023 pekee, idadi kubwa ya watalii walioingia nchini walitoka Italia (14,986), Marekani (14,416), Ufaransa (11,997), Uingereza (9,852) na Ujerumani (9,161).

4.2 Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Kutoka Bara la Afrika

Katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2023, Tanzania ilipokea pia watalii kutoka katika Bara la Afrika, ambapo idadi kubwa ya watalii walitoka Kenya (128,753), Burundi (69,505), Zambia (38,394), Rwanda (37,269) na Uganda (28,594). Aidha, katika kipindi cha mwezi Agosti 2023 pekee idadi kubwa ya watalii walioingia nchini walitoka Kenya (18,550), Burundi (12,310), Zambia (6,649), Rwanda (5,124) na Uganda (4,052).

5.0 Hitimisho

Sekta ya Utalii ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya fedha za kigeni nchini, hivyo taasisi na kampuni zinazotoa huduma kwa watalii zinatakiwa kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa lengo la kuvutia watalii wapya na wanaokuja nchini kwa mara nyingine.

Kwa mujibu wa Sera ya Mapitio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu za idadi ya watalii wanaoingia nchini zinaweza kufanyiwa mapitio endapo takwimu mpya na zilizohuishwa kutoka kwenye chanzo zitapatikana.



Kwa taarifa zaidi wasiliana na Mtakwimu Mkuu wa Serikali
S.L.P 2683 Dodoma,
Simu +255 26 2963822, Nukushi +255 26 296382,
Barua pepe: sg@nbs.go.tz, tovuti: www.nbs.go.tz